**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA OLD MOSHI.**

**Namba za simu:**
0 716 183 232 **Mkuu wa shule**
0 629 771 624 **Mkuu wa shule**
0 753 659 834 **Makamu mkuu wa shule**.
**0 699 776 618 Mwalimu Mlezi wa wanafunzi**

**SHULE YA SEKONDARI OLD MOSHI,**
**S.L.P 1996**,
**MOSHI**.
**JUNI, 2024**

**MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI** ______________________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA OLD MOSHI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2024-2025.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika ya **sekondari ya wasichana OLD MOSHI** mwaka 2024-2025 na atasoma tahasusi ya **_____** . Shule ya sekondari **OLD MOSHI** ipo mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya ***Moshi***, kata ya ***Old Moshi Mashariki***, katika Kijiji cha ***Tsuduni***, umbali wa **kilomita** 14**,** kutoka stendi kuu ya Moshi mjini. Usafiri kutoka Moshi mjini hadi kufika shule (*Haisi zinapatikana standi ya moshi mjini*, *unapanda haisi zinazoenda* ***Mjohoroni***, *Unashuka kituo kinaitwa* ***Kiboroloni shule*** *– Nauli ni Sh. 600, Kisha unapanda Pikipiki hadi shuleni (Nauli ni sh. 2000 tu*). Pia unaweza kukodi bajaji kutoka stendi kuu hadi shuleni (Nauli isizidi 10,000)

Muhula wa masomo unaanza tarehe **___/___/2024** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **___/___/2024** na mwisho wa kuripoti ni Tarehe **___/___/2024**.

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**KUNDI A: MICHANGO MBALIMBALI**

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 01 | Mchango wa uendeshaji wa shule | Tsh. 65,000/= |
| 02 | Tahadhari | Tsh. 5,000/= |
| 03 | Nembo | Tsh. 5,000/= |
| 04 | Kitambulisho cha shule | Tsh. 5,000/= |
| **JUMLA KUU** | | **TSH 80,000/=** |

❖ Pamoja na barua hii viambatanisho vifuatavyo vimefungashwa:

i. Kiambatanisho A: Sheria za shule (*ukurasa wa* 3)
ii. Mshono wa sare ya shule (ukurasa wa 4)
iii. Baadhi ya vitabu unavyoweza kumnunulia mwanao (*ukurasa wa* 5&6)
iv. Kiambatanisho B: Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi (*ukurasa wa* 7)
v. Kiambatanisho C: Fomu ya daktari (*ukurasa wa* 8) **ijazwe na lazima iwe na muhuri wa daktari**.
vi. Kiambatanisho D: Ahadi ya mzazi /mlezi kumuhudumia mwanafunzi na Ahadi ya utii na tabia njema kwa mwanfunzi (*ukurasa wa* 9)

***NB:*** *Michango yote ilipwe kwenye akaunti NA:* ________________ *jina la akaunti ni* ______________________

HEADMISTRESS
OLD MOSHI GIRLS SECONDARY
P. O. Box 1996, MOSHI

**REHEMA ISAAC**
**MKUU WA SHULE**

## KUNDI B: <u>SARE ZA SHULE.</u>

### SARE YA DARASANI.

- **i.** Sketi mbili (**02**) rangi ya **Dark Blue** zenye rinda box la upana wa inchi nane na sketi iwe ndefu kabisa hadi miguuni (kwenye kifundo cha miguu)**. Zingatia maelekezo kuepuka usumbufu wa kushona upya uniform.**
- **ii.** Shati mbili nyeupe za mikono Mirefu kwa wote. Kwa waislamu aje na HIJABU NDEFU YA KITAMBAA CHA HALUA (**Hijabu/shungi iwe ndefu inayofunika mikono yote).** Hijabu fupi na isiyo ya **Halua** hairuhusiwi.
- **iii.** Sweta mbili za rangi ya **Dark Blue.**
- **iv.** Viatu vyeusi vya ngozi vyenye Kamba (gidamu) vya kufunika miguu, (**mashimo ya kamba kuanzia manne kila upande**) kisigino kifupi na visiwe na mapambo yoyote. (Mabuti, *Travota, Bova,Viatu vingine vyenye mapambo na viatu vilivyo na matundu ya kamba pungufu ya manne***, HAVIRUHUSIWI KAMA SARE YA SHULE HIVYO ASIJE NAVYO**)
- **v.** Aje na soksi rangi nyeupe **fupi**, jozi mbili
- **vi.** Tai ndefu rangi ya **Dark Blue**. (Rangi ya Sketi)

### SARE YA KUSHINDIA.

- i. Sketi mbili rangi ya Brown (ugoro) zenye rinda box la upana wa inchi nane sketi iwe ndefu kabisa hadi miguuni**,** na T-shirt mbili (02) za **Light blue, Zenye kola (*for six*)** zisizo na maandishi yoyote, Sare hii ni **kwa ajili ya kushindia**.
- ii. Kwa waislamu **hijabu** za kushindia na "***vya kuvalia ndani ya hijabu***" ni rangi **nyeupe tu**, visiwe na urembo wowote. **Hijabu iwe ya halua ndefu inayofunika mikono yote.** Atavaa awapo darasani na hata katika sare ya kushindia.
- **iii.** Aje na track suti rangi ya **Dark bluu** kwa ajili ya kuvaa wakati wa kujisomea usiku. Kwa walio na tatizo wakati wa baridi unaruhusiwa kuja na sweta aina ya "***prue neck/kaba shingo***" nyeupe au nyeusi itavaliwa ndani ya shati la shule.
- **iv.** Aje na yeboyebo nzito zinazohimili matope kwa wakati wa mvua tu.

### SARE ZA MICHEZO.

- **i.** Kila mwanafunzi aje na bukta na tshirt rangi ya nyeusi (*jezi ya Taifa stars*) raba nyeupe isiyo na mapambo yoyote wala isiwe imechanganywa rangi kwa ajili ya michezo tu.

**NB:** ***Kwa wale watakaohitaji, Uniform Kushonea shuleni. Wasiliana na makamu mkuu wa shule kupata utaratibu. (Namba imeandikwa juu uk.1)***

**KUNDI C: Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

1. Madaftari makubwa (counter book) ya kutosha masomo yake, mazoezi na majaribio.
2. Ream ya karatasi **(A4) -** mbili (2) na Rimu Ruled moja (1) kwa mwaka.
3. Kalamu za kutosha za wino, penseli, ufutio, stapler mashine na stapler pins.
4. Scientific Calculator, kwa wanaosoma masomo ya (Eonomics, Geography, Physics na Mathematics)
5. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika. (**vimeorodheshwa uk. wa 05-06**)
6. Godoro la inchi $2^{1}/_{2}$ x 6, Shuka 2 za rangi ya pinki, Chandarua rangi nyeupe, Blanketi, Ndoo ndogo ya kuogea, Sanduku dogo la chuma, (asije na begi la nguo, sanduku la chuma yaani tranka linatosha.) Mto na foronya za pinki, Torch na betri, Vyombo vya chakula, bakuli (container) kijiko na kikombe.
7. Aje na mahitaji yake binafsi kama mafuta, mswaki dawa ya meno, sabuni n.k (manukato ya namna yoyote hayaruhusiwi) Pia anaruhusiwa kuja na vitabu vya dini kulingana na Imani yake Mfano; (Biblia Takatifu, Mwimbieni Bwana, Rozali, Quran Tukufu, Tasbihi)

**VIFAA VYA USAFI – KILA MWANAFUNZI ALETE KUTOKANA NA TAHASUSI (COMBINATION) YAKE**;

| EGM | HGL | HKL | PCM |
|---|---|---|---|
| - Jembe lenye mpini<br>- Panga moja<br>- Toilet brush<br>- Ufagio wa chelewa wenye kishikio cha mti. | - Jembe lenye mpini<br>- Kwanja/Slasher<br>- Soft broom<br>- Hard broom<br>- Reki ya chuma | - Dawa/Sabuni ya chooni lita tano (**05 ltrs)**<br>- Kwanja/Slasher<br>- Ndoo kubwa ya lita 20.<br>- Squizer/Moper moja | - Jembe lenye mpini.<br>- Ufagio wa chelewa wenye kishikio cha mti.<br>- Squizer/Moper moja<br>- Fagio wa buibui |

**vifaa vyote vikabidhiwe ofisini utakapopokelewa.**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOTAJWA JUU KABISA

**KIAMBATANISHO: A**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shule.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**)


## MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA;


i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. (***Kwa namna yoyote ile shuleni kwetu wanafunzi hawasuki nywele***) hivyo mwanafunzi awe na nywele fupi.
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kusababisha mimba.
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu, na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA OLD MOSHI SEKONDARI.**

**SAMPULI YA MUONEKANO WA SKETI YA SHULE**





NB: **Mzazi unashauriwa kumnunulia mwanao baadhi ya vitabu atakavyohitaji kulingana na tahasusi aliyochaguliwa. Mfano wa vitabu hivyo vimeorodheshwa katika jedwali lifuatalo;**

| Na. | SOMO | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| 1. | ENGLISH LANGUAGE | - Oxford Advanced Learner's Dictionary<br>- Advanced Level English: A Practical Aproach. Nicholaus Asheli,Good Book Publishers<br>- Literature for advanced level: Godfrey Ruta Bukagile.Nyambari Nyangwine Publishers<br>- English for A level - Oxford<br>- English For Form 5&6 Phonology Part II; Michael Kadeghe.<br>- Complete English Course For Form 5&6 students; Michael Kadeghe<br>- Advance Level English Language, PP II (Novel Questions and Answers; Nyambari Nyangwine |
| 2. | KISWAHILI | - Massamba D.P () Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu TUKI, Dar es salaam.<br>- Massamba D.P na wenzake () Sarufi miundo ya kiswahili sanifu TUKI, Dar<br>- es salaam.<br>**RIWAAYA**<br>- Vuta ni kuvute Mkuki na Nyota publishers LTD, Dar es Salaam, Shafi Adam (1999).<br>- Usiku utakapokwisha Macmillan Aidan LTS Dar es Salaam, Msakile . Mbunda (2007).<br>- Mfadhili Macmillan Aidan LTD Dar es Salaam, Tuwa Hussein (2007).<br>- kufikirika. Oxford University Press Nairobi, Robert . S.<br>**TAMTHILIYA**<br>- kwenye ukingo wa Thim Oxford University Press, Hussein Ebrahim (1988)<br>- Kivuli Kinaishi Oxford University Press Nairobi, Mohamed .S. (1990).<br>- Nguzo Mama Macmillan Aidan LTD Dar es Salaam, Muhando P. (2007).<br>- Morani. Macmillan Aidan LTD Dar es Salaam, Mbogo Emmanuel ( 2007).<br>**USHAIRI**<br>- Chungu Tamu T.P.H Dar es salaam, Mvungi T. (1985)<br>- Fungate ya Uhuru Macmillan Aidan LTD Dar es Salaam Khatibu S. (2007)<br>- Kimbuga TUKI Dar es Salaam, Haji Gora ( 2001).<br>- Mapenzi Bora Mkuki na Nyota Publishers Dar es Salaam Rober S. ( ). |
| 3. | HISTORY | - Mastering Modern World History- Norman Lowe<br>- How Europe Underdeveloped Africa-Walter Rodney<br>- Problems and Prospective in History; Social Changes and Revolution in England 1540-1640; Lawrence Stone<br>- Adv. Level History Qns and Ans; Nyambari Nyangwine<br>- The Origins and Development of Africa societies selected Qns and Ans; Nyambari Nyangwine<br>- A History Modern Europe 1789-1981; H. L. Peacock |
| 4. | GEOGRAPHY | - Integrated Approach to Physical Geography (Msabila)<br>- Integrated Geography (By F. J. Monkhouse)<br>- Map reading for East Africa<br>- Principles of Geography (By F.J. Monk house)<br>- **General Geography in diagram (By R.P. Bunnet)**<br>- Simplified Physical Geography for a level (By D.M.Mapunda)<br>- Practical Geography For Africa (Longman 1983) J. M. Pritchard<br>- Atls For Secondary schools; Longman Group<br>- **Geography, An Intergrated Approach; D. Waugh**<br>- An Integrated Focal Reginal Studies on Human Economic Geography; A-Level PP 1&2 D. T. Msabila |
| 5. | ECONOMMICS | - Modern Economics by Hardwick 4th Ed<br>- Simplified Economics. N. A. Salemi<br>- Managerial economics. N.kazi njema Mama |
| 6. | PHYSICS | - Nelkon and Parker<br>- Understanding Physics.<br>- Rodger Manchester.<br>- Calculation for A-level |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | CHEMISTRY | - Organic Chemistry Volume I<br>- Advanced level Inorganic chemistry Part I & II (TIE 1995)<br>- Advanced Chemistry review by William W. Davis (Mzumbe Book Project 2004)<br>- Physical Chemistry by Delungu (Mzumbe Book Project, 1998)<br>- Chemistry in Action; Freementle M<br>- A-Level Physical Chemistry; Heys 6th Edition<br>- A-Level Chemistry; E.N Ramsed |
| 8. | MATHEMATICS | - Advanced Mathematics Form V, VI by gdy publishers<br>- Understanding pure mathematics by chandler.<br>- Advanced level pure mathematics by C. J Tranter.<br>- Advanced Mathematics volume I and II (Ministry of Education and Vocational Training)<br>- Pure mathematics Vol. I & II by Back House |

**WAZAZII, WALEZI NA WAGENI;**

Wazazi/Walezi na wageni watawaona wanafunzi siku ya kikao cha wazazi/walezi na siku za mahafali. Mzazi usishtushwe na barua za mwanao au kupata taarifa isiyo rasmi. Iwapo lipo tatizo uongozi wa Shule utakujulisha Ikiwa kuna shida muhimu mfano msiba wa baba/mama au mlezi kisheria taarifa iletwe kwa uongozi wa Shule kuwepo na uthibitisho wa kifo mfano barua ya Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa. Hii ni kudhibiti ulaghai wa baadhi ya watu wachache wanaotumia mianya hiyo kuwapotezea wanafunzi muda wa kusoma.

Wazazi/Walezi wanaruhusiwa kuwaona wanafunzi siku ya Kikao cha wazazi/walezi ambacho hufanyika mara moja kwa mwaka. Tarehe kamili utajulishwa.

**<u>KIAMBATANISHO:</u> B**

| BANDIKA PICHA (PASSPORT SIZE) YA MWANAFUNZI HAPA |
|---|

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI.**

| **NA** | **MAELEKEZO** | **JAZA TAARIFA HAPA** |
|---|---|---|
| A. | JINA KAMILI: (Majina matatu kama yalivyosomeka katika mitihani wa Taifa) | |
| B. | TAREHE YA KUZALIWA: | |
| C. | KABILA: | |
| D. | MKOA ALIPOZALIWA: | |
| E. | WILAYA ALIYOZALIWA: | |
| F. | JINA LA MZAZI: | |
| G. | KAZI YA MZAZI/MLEZI: | |
| H. | NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI: | |
| I. | WAZAZI WAPO PAMOJA AU WAMETENGANA: | |
| J. | MAMA YUPO HAI? (Ndiyo/Hapana) | |
| K. | BABA YUPO HAI? (Ndiyo/Hapana) | |
| L. | SHULE YA MSINGI ALIYOTOKEA MWANAFUNZI: (SHULE - WILAYA - MKOA) | |
| M. | SHULE YA SEKONDARI (O-LEVEL) ALIYOTOKEA MWANAFUNZI: (SHULE - WILAYA - MKOA): | |
| N. | NAMBA YA SIMU YA NDUGU WA KARIBU WAKATI WA DHARURA: | |
| O. | UHUSIANO WAKE (**NDUGU WA KARIBU**) NA MWANAFUNZI: | |
| P. | TATIZO LA KUDUMU LA KIAFYA KAMA LIPO. (***Lithibitishwe na VIPIMO vya daktari katika fomu ya daktari kwenye kiambatisho C)*** | |
| Q. | SAINI YA MWANAFUNZI: | |
| R. | SAINI YA MZAZI/MLEZI: | |
| S. | HAPA JAZA NAMBA YA SIMU AMBAYO INAPATIKANA **WHATSAPP** AMBAPO TAARIFA ZA MWANAFUNZI ZITATUMWA IKIWA NI PAMOJA NA MATOKEO. **(NI LAZIMA**) ________________ | |
| | **KWA MATUMIZI YA OFISI TU.** | |
| A. | MKONDO NA DARASA ALIPOPANGIWA MWANAFUNZI: | |
| B. | SAINI YA MWALIMU WA DARASA: | |
| C. | SAINI YA MKUU WA SHULE: | |
| D. | TAREHE: | |
| E. | MUHURI WA OFISI: | |

**KIAMBATANISHO:** **C**

**PRRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION LOCAL GOVERNMENTS**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**

**OLD MOSHI GIRLS SECONDARY SCHOOL,**
**P.O. BOX 3003,**
**MOSHI.**

**Date ____________**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.**

**TO THE MEDICAL OFFICER.**

Please ________________________________________ (name of the student) who has been selected to join this school for his/her fitness as a student in the following areas (to be completed by a medical officer)

1. Eye sight __________________________________________
2. Hearing __________________________________________
3. Tuberculosis (T.B) __________________________________________
4. Specimen __________________________________________
   i. Stool __________________________________________
   ii. Urine __________________________________________
   iii. Blood __________________________________________
5. Asthma __________________________________________
6. Pregnancy __________________________________________
7. Other diseases/ any disabilities ______________________________________________________________
   ____________________________________________________________________________________________________

**MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by medical officer.)

I have examined the above named and consider that he/ she is physically not physically fit as a student.

***Date* __________________** ***Signature* ______________________________**

***Station* __________________** ***Designation* ____________________________**

***Official stamp* _______________________________**

***NB: I request this form to be returned to the school in a sealed envelope***

**KIAMBATANISHO: D**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI.**
**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA OLD MOSHI**

**AHADI YA UTII / TABIA NJEMA.**

Mimi ________________________________________________________ (*majina matatu ya mwanafunzi*) ninayejiunga kidato cha __________________ katika shule ya sekondari ya wasichana Old Moshi, natambua vyema wajibu wangu kwa taifa kama mwanafunzi, kwa hiyo naahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu na mbele ya Mkuu wa shule kuwa :-

a. Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote halali yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
b. Nitatii na kuwaheshimu walimu, watumishi wasio walimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya viranja wa madarasa, viranja wa shule, walimu, watumishi wasio walimu hadi mkuu wa shule.
c. Na kama nitashindwa kufuata/kuzingatia maadili mema nipewayo na walimu wangu shuleni hatua kali zitachukuliwa dhidi yangu ambayo ni pamoja na kufukuzwa shule.

**Saini ya Mwanafunzi ______________________________________ Tarehe _______________________**

**AHADI YA MZAZI YA KUMUHUDUMIA MTOTO NA KUTEKELEZA WAJIBU WAKE KAMA MZAZI/MLEZI.**

Mimi __________________________________________________________________ Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ____________________________________________ wa kidato cha ________________
Ninakubali/Sikubali kuwa mtoto wangu ajiunge na shule ya sekondari ya wasichana Old Moshi kuanzia leo tarehe _________________ na naahidi kuwa nipo tayari kumuhudumia mtoto kwa kila jambo linalonihusu kama Mzazi/mlezi. Aidha naahidi kuwa Nitafuatilia maendeleo ya mwanangu awapo shuleni, na mtoto wangu ameahidi mbele yangu kuwa atakuwa mtiifu na mwenye bidii awapo shuleni.

Ninatambua uwepo wa dini mbalimbali, na nikiwa kama Mzazi/Mlezi ninapenda mtoto wangu akiwa shule alelewe katika dini ya ______________________________ dhehebu ____________________________

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi ______________ Tarehe _______________ simu No: _________________________**

**SEHEMU HII NI KWA AJILI YA OFISI TU.**

**Maoni ya mkuu wa shule: ____________________________________________________________________**

______________________________________________________________________________________

**Saini ya Mkuu wa Shule. ____________________________________ Tarehe: ___________________**